# COUNTY ASSEMBLY OF SAMBURU

***THE HANSARD***

**Tuesday, 20th May, 2025**

**The Assembly met at the County Assembly Chambers at 2:30 pm**

***The Speaker, (Mr. Lenamarle Stephen) in Chair***

## PRAYER

Disclaimer: The electronic version of this Hansard report is for information purposes only. A certified copy can be obtained from the Hansard Editor, County Assembly of Samburu. 

## QUESTIONS AND STATEMENTS

EARLY CHILDHOOD DEVELOPMENT

TEACHER'S RECRUITMENT 2024

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Hon. Members, it is notified that the following statement is due for response today Tuesda 20th May, 2025 at 2:30 PM Pursuant to Standing Order 52 (b):

1. Statement No. 003/2025; requested by Hon. Esther Lonolkulal; MCA. To the Chairperson Sectoral Committee on Public Service and Administration, Social Welfare, Labour, Justice and Legal Affairs, regarding the teacher's recruitment on Early Childhood Development Education(ECD)

**Chairperson Committee on Public Service and Administration, Social Welfare, Labour, Justice and Legal Affairs,** (Hon. Leleruk James): Ahasante Mheshimiwa Spika. Nataka kusoma taarifa iliyotumwa kwa ajili ya swali la Mheshimiwa Esther.

Halmashauri ya Uajiri ya Kaunti ya Samburu imepokea ombi lako la taarifa lililorejelewa ka SBU/CK/SCPRT/VOL.I/01/2025 la tarehe 12 Mei, 2025; ambapo Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma kwa Uma na Utawala, Ustawi wa Jamii, Haki na Masuala ya Kisheria alitaka kufahamu kutoka kwa Halmashauri kuhusu yafuatayo kuhusiana na ajira ya walimu wa ECDE DARAJA LA TATU KATIKA Kaunti ya Samburu:

1. Walimu wote wa ECDE Teacher III walioorodheshwa wakati wa mchakato wa kuajiri mwezi Agosti, 2024.
2. Maelezo ya kucheleweshwa kwa tangazo ya walimu waliofaulu, ambalo lilifanywa mwishoni Januari, 2025 baada ya kufanya mahojiano Agosti, 2024?
3. Habari kuhusu hatua ambazo Idara ya elimu ya Kaunti imechukuwa kwa walimu wa ECDE waliohitimu lakini hawakufanikiwa kupata nafasi ya kuajiriwa katika Kaunti ya Samburu.
4. Jinsi jitihada za uajiri zimegawanywa kwa usawa katika kata zote Kumi na Tano Kaunti ya Samburu, na pia kuhakikisha ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu.

Haya ndiyo majibu kuhusu ombi la tamko juu ya uajiri wa walimu wa ECDE katika serikali ya Kaunti ya Samburu na Halmashauri ya Uajiri ya Kaunti ya Samburu

Ombi la Kwanza (1): Walimu wote wa ECDE Teacher III walioorodheshwa wakati wa Mchakato wa kuajiri mwezi Agosti, 2024.

Tangazo la Ajira kwa Ajira ya walimu wa ECDE lilitolewa ba Bodi ya Kaunti tarehe 31 Oktoba, 2023. Tangu wakati huo, Katibu/Mkurugenzi Mtendaji alijiuzulu kazini na Katibu/Mkurugenzi Mtendaji mpya aliteuliwa tarehe 2 Julai, 2024. Uteuzi wa awali (shortlisting) na usaili wa walimu wa ECDE ulifanyika kuanzia tarehe 19 Agosti, 2024 hadi 5 Septemba, 2024. Wafuatao waliteuliwa kwa usaili na waliofanya usaili kama inavyoonyehwa kwenye jedwali hapa chini.

Mhesimiwa Spika sitasoma majina yote kwasababu najua kwamba kila Mheshimiwa amepata majina ya walimu wote walioorodheshwa kwa Wadi kulingana na Jinsia, Umri na kama mtu ni ama si mlemavu.

Walimu wote walioorodheshwa ni 332

Swali la Pili (2): Maelezo ya kucheleweshwa kwa tangazo ya walimu waliofaulu, ambalo lilifanywa mwishoni Januari, 2025 baada ya kufanya mahojiano Agosti, 2024.

Kwa heshima kubwa, tungependa kuwapa taarifa ifuatayo kuhusiana na kucheleweshwa kwa kutangazwa kwa majina ya walimu wa ECDE waliofaulu katika mchakato wa ajira uliofanywa na Idara ya Uajiri ya Kaunti mwishoni mwa mwezi wa Januari 2025, baada ya mahojiano yaliyofanyika mwezi Agosti 2024:

1. Uchambuzi wa mwisho wa matokeo:

Baada ya kukamilika kwa mchakato wa mahojiano, kulihitajika muda wa ziada kwa ajili ya kuchambua matokeo kwa kina ili kuhakikisha haki, usawa na uwazi kwa kila mgombea. Tumejizatiti kuhakikisha kuwa orodha ya waliochaguliwa inazingatia vigezo vilivyowekwa.

2. Ukaguzi na uthibitisho wa nafasi:

Idara husika ya Kaunti ililazimika kufanya uthibitisho wa nafasi zilizopo, ikiwemo uhakika wa bajeti, idadi ya vituo vya ECDE vinavyohitaji walimu, na vigezo vya usambazaji wa rasilimali watu katika maeneo mbalimbali.

3. Uhakiki wa vyeti na taarifa binafsi:

Kabla ya kutangaza majina ya waliofaulu, Idara YA Kaunti ilikuwa ikifanya uhakika wa vyeti na taarifa binafsi za wagombea ili kuzuia udanganyifu na kuhakikisha kuwa wote waliofaulu wanakidhi masharti yaliowekwa kisheria.

4. Mtihani wa ustahiki kwa ajili ya kupandishwa viwango kwa Wafanyikazi wa Afya KATIKA Idara ya Afya

Mara tu baada ya Bodi ya Kaunti kukamilisha usaili wa Walimu wa ECDE, mitihani ya ustahiki wa Wafanyakazi mbalimbali wa Afya ilipangwa kufanyika kuanzia tarehe 9 Oktoba, 2024 hadi tarehe 11 Oktoba, 2024, na barua za kupandishwa vyeo zilitolewa tarehe 24 Oktoba, 2024. Hili lilisababisha kucheleweshwa kwa kutolewa kwa orodha ya wagombea waliofaulu kwa ajili ya kujaza nafasi za walimu wa ECDE.

Ombi la Tatu (3): Habari kuhusu hatua ambazo Idara ya elimu ya Kaunti imechukuwa kwa walimu wa ECDE waliohitimu lakini hawakufanikiwa kupata nafasi ya kuajiriwa katika Kaunti ya Samburu:

Idara wa Elimu ya Kaunti ya Samburu inatambua mchango mkubwa wa walimu wa ECDE waliohitimu katika maendeleo ya elimu ya awali katika jamii yetu. Tunafahamu kuwa kuna idadi kubwa ya walimu waliomaliza mafunzo yao kwa mafanikio lakini hawakupata nafasi za ajira katika mchakato wa hivi karibuni.

Kwa kutambua hali hii, Idara ya Elimu ya Kaunti imechukuwa hatua zifuatazo:

1) Kutenga fedha maalum kwenye bajeti kila mwaka kwa ajili ya kuajiri walimu wapya wa ECDE;

Kuweka fedha maalum kila mwaka kwenye bajeti kwa ajili ya Idara ya Elimu hasa kwa sekta ya Walimu wa ECDE, kunaweza kusaidia kuipunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa walimu wa ECDE katika Kaunti ya Samburu.

Fedha zilizotengewa katika bajeti zinaweza kutumika kuajiri walimu wapya wa ECDE kwa mkataba au kudumu, hivyo kuongeza nafasi za ajira kwa walimu waliomaliza mafunzo lakini hawana kazi.

2) Kuandikisha walimu wote waliohitimu kwenye hifadhidata ya Kaunti:

Ili kuhakikisha kuwa walimu wote waliohitimu hawasahauliki katika mchakato wa ajira zijazo, Idara imetengeneza hifadhidata rasmi ya walimu wa ECDE waliokosa ajira kwa sasa. Hii itasaidia kuwaweka katika orodha ya kwanza ya kuzingatiwa endapo nafasi mpya zitapatikana au pale walimu wa sasa watakapostaafu au kuhama.

3) Mpango wa ajira ya mkataba kwa muda mfupi (internship)

Kaunti inapanga kuanzisha mpango wa ajira ya muda kwa msingi wa kujitolea au internship, ambapo walimu wa ECDE waliohitimu wanaweza kufanya kazi kwa muda maalum huku wakilipwa marupurupu. Hii inalenga kuwapa uzoefu wa kazi na kuwapa kipaumbele katika ajira za baadaye.

4) Ushauri na mwongozo kwa walimu kuhusu fursa mbadala:

Idara pia inawashauri walimu waliohitimu kuchunguza fursa mbadala kama vile kuanzisha vituo binafsi vya ECDE au kuomba kazi katika Kaunti jirani ambazo zina upungufu wa walimu.

Idara pia inaendelea kufanya juhudi kuhakikisha kuwa kila mwalimu aliyehitimu anapata nafasi ya kutoa huduma yake kwa jamii. Tunaomba walimu waendelee kuwa na subira na kujiandaa kutumia fursa zitakazojitokeza.

Ombi la Nne (4): Jinsi jitihada za uajiri zimegawanywa kwa usawa katika kata zote Kumi na Tano Kaunti ya Samburu, na pia kuhakikisha ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu.

Serikali ya Kaunti ya Samburu kupitia Idara ya Uajiri imetekeleza mchakato wa ajira wa walimu wa ECDE kwa kuzingatia misingi ya usawa wa kieneo na ujumuishaji wa makundi maalum kama vile watu wenye ulemavu. Hili limefanyika kwa njia zifuatazo:

1. Usawa wa Kieneo kati ya Kata zote 15.

1) Ugawaji wa nafasi kwa misingi ya kila Kata: Idara ya Uajiri ilifanya uhakika wa mahitaji ya walimu katika kila Kata kabla ya kutangaza nafasi ili kuhakikisha kila Kata inapata walimu kulingana na idadi ya vituo vya ECDE vilivyopo na uhaba wa walimu.

2) Uwiano wa nafasi za ajira: Katika mgao wa nafasi, kila kata kati ya 15 ilitengewa nafasi kwa uwiano unaozingatia idadi ya Wanafunzi, upatikanaji wa miundombinu ya ECDE na walimu waliopo.
3) Uwakilishi wa jamii mbalimbali: Mchakato umehakikisha Kata zote zinapata uwakilishi wa moja kwa moja huku kipaumbele kikitolewa kwa waombaji waliotoka katika maeneo husika ili kukuza huduma za elimu kijumuiya.

2. Ujumuishwaji wa Watu wa ulemavu (PWDs)
   1) Nafasi maalum kwa watu wenye ulemavu: Serikali ya Kaunti imetenga asilimia maalum ya nafasi kwa ajili ya watu wenye ulemavu kwa mujibu wa sera za kitaifa na miongozo ya Tume ya Huduma za Uma.
   2) Upendeleo chanya katika uteuzi: Katika mchakato wa uteuzi, waombaji wenye ulemavu walipewa kipaumbele kwa sifa zinazolingana na kuwezeshwa kwa ajili ya mazingira Rafiki wakati wa mahojiano.
   3) Uhakiki wa hali ya ulemavu: Wote waliodai kuwa na ulemavu walihitajika kuwasilisha vyeti halali kutoka kwa Daktari Mkuu wa wa Serikali au Bodi ya walemavu ili kuhakikisha uwazi na usahihi wa taarifa.

Kwa kuzingatia misingi haya, Serikali ya Kaunti ya Samburu inajivunia kuwa katika mstari wa mbele katika kuhakikisha usawa wa kieneo na ujumuishwaji wa makundi maalum katika utoaji wa huduma za elimu ya awali ya watoto.

Mheshimiwa Spika, jedwali ya pili (2) ni oradha ya majina ya watahiniwa waliofaulu kuchukua nafasi ya walimu wa ECDE daraja la tatu mwaka 2024, Nafikiri Waheshimiwa mnaona hiyo orodha ya watu hamsini na wanne wale ambao waliteuliwa waliweza kufanya nafasi ya walimu wa ECD daranja ya tatu walio faulu kuchukua ni hamsini na nne nafikiri kila mtu ataweza kusoma n kuona wametoka Wadi gani. Jedwali ya tatu watahiniwa walio faulu kuwa walimu wa ECD mwezi wa Februari 2025. Kuna orodha hilo pia ya walimu walioajiriwa Februari 2025 na kuna wale ambao nafasi walio faulu mwaka wa 2024 54 na orodha lingine la 50. Mtaangalia na hii ni uchambuzi wa waliotahiniwa waliofaulu katika elimu ya maendeleo ya awali ya mtoto wa ECD kwa mwezi wa Januari na Februari 2025 watahiniwa waliofaulu katika elimu ya maendeleo

ya awali ya watoto wa ECD kwa kuzingatia Wadi na jinsia ni asilimia ya jumla. Samburu North kuna wa kiume na kike na idadi yake ni kama 32, Samburu Central 51, Samburu East 21.

Jedwali la tano; asilimia za jumla za uteuzi wa mafunzo ya elimu ya awali kwa watoto wa ECD wa kwa kila Tarafi Sub County Samburu North wale wa kike ni 50 wa kiume ni 49 kwa jumla ni 99. Sambur Central wa kike ni mia moja na tatu wa kiume ni 67 wote ni 170 ni asilimia 51% Samburu East wa kike ni 32 wa kiume ni 27, 59 Asilimia 17 wale wengine wa kike walikua wanne jumala yote ni mia moja na wenye ulemavu 6 kati ya 104 wakapata ni 5.8. Hayo ndio majibu ambayo nimeweza kuwakilisha kutoka kwa idara ya Labour.

**Specially Elected MCA,** (Hon. Lenolkulal Esther): Asante Mheshimiwa Spika. Namshukuru mwenyekiti ambaye amejaribu kujibu hoja langu Niliuliza nikiwa najua walimu 53 waliajiriwa na pia nimepata jibu kuwa wa;imu pia waliajiriwa 2024/2025 na swali langu liliulizaya 2024 ya walimu 53 kuajiriwa. Sikujua pia kuna walimu waliajiriwa mwaka huu Mheshimiwa Spika ningetaka maelezo zaidi kwasababu sijawahi kuona tangazo ya kuajiri walimu walio ajiriwa mwaka huu ingawa nimepata ripoti wako nilikuwa nimeuliza kwasababu nataka kujua kwa Wadi zote kama wamepata usawa.

Vile wamejibu hapa naona kama kila Wadi limepata kwa usawa kulingana na majibu ingawa sina uhakika. Nimeona pia walemavu sita wameajiriwa kati ya 104 ambayo ni idadi ndogo sana na kati yao wawili ni wamama ambayo ni idadi ndogo sana na wakiajiri tena naomba waongezwe kwani wako na idadi kubwa katika Kaunti letu. Swali langu ni hao walimu wa 2025 walitangazwa wapi na niliuliza nikujua walimu ni 53 walioajiriwa ambayo tuliona kwa hii Nyumba au kwa taarifa. Tunataka uajiri utangazwe ili watu wetu waweze kutafuta kazi.

Watu wengi wamesomea hii kazi ya walimu, ukiangalia hapa ni zaidi ya watu zaidi ya mia tatu. Naomba itangazwe ili tuwe na usawa. Nashukuru Mwenyekiti kwasababu angalau kina mama wameangaliwa leo sitapiga kelele sana. Nataka kujua hao walimu waliandikwa linin a walitangazwa wapi, ahsante.

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Mheshimiwa Leleruk nataka ufafanue zaidi walimu waliajiriwa mwaka gani kama kuna wale wameajiriwa mwaka huu ama mwaka ujao. Fafanua kidogo ili Mheshiwa Esther arithike.

**Chairperson, Committee on Labour,** (Hon. Leleruk James): Mheshimiwa Spika naona Mheshimiwa Esther amerithika na nilikuwa nimemuonyesha ingawa analalamika hawa walimu wengine hamsini waliandikiwa kwa njia gani na naona yeye alipata nafasi kubwa hapa Central yeye ndiye anaongoza na ndiyo kwasababu hataki kuongea ile ambaye ilikua imetangazwa ni wale watu kati ya 54 ile ya kwanza ilikuwa kama kubadilisha na kunai le ingine idara waliongeza ili iwe 54 na hii ingine pia mimi kama Mwenyekiti wa Labour niliweza niliweza kuuliza na silalamiki, ukiangalia kwa Wadi zote Wadi ya Suguta ndio ilipata nafasi mbili kati ya ile hamsini na sina nyongo kwasababu nimeona wale ambao walichukuliwa kwa nini haijatangazwa kwasababu Mheshimiwa Esther alikuwa ameuliza hawa walimu wengine watafanyiwa nini.

Haikutangazwa kwasababu tayari walimu 332 walitahiniwa lakini hawakufaulu lakini hawa wengine 50 ambaye tunataka kupongeza nataka kama nyumba tuweze kupongeza idara ya uajiri kwa kufanya mbinu zao na kuongeza nafasi hamsini na ndio kwasababu hawakuweza kutangazwa, tayari tuko na walimu zaidi 332 ambaye tayari wako na makaratasi, wamepita mtihani lakini hakuna vile watafanyiwa.

Ile orotha ya 332 ndio nafasi hizo zilitolewa, ukiangalia kwa kiini ni wale tu waliorothewa kuwa wametahiniwa na ndio tunapongeza idara ya uajiri kwa kazi nzuri, kila mtu anaona na kila kitu iko wazi Kwa upande wa ulemavu kama vile ameuliza nataka kupongeza idara kwa sababu kwa orodha ya 332 inaonyesha mlemavu na kama kuna wale wameachwa najua tutaweza kufuatilia, asante.

**Specially Elected MCA,** (Hon. Osman Dube): Asante sana Mheshimiwa pika. Shukrani yangu ya kwanza ni kwa Mheshimiwa Esther kwa mambo mawili, kwanza ni uajiri nay a pili leo Bunge linazungumza Kiswahili pekee yake nay a tatu leo Bodi ya uajiri wameandika kwa Kiswahili, ujuzi kubwa sana. Napongeza mwenyekiti kwa kujibu swali vyema kwa sababu yote aliyosoma nimefuatilia tangu ufutiliaji mbali ya uajiri wa walimu ya kwanza. Sisi sio living with disability lakini ni kasoro kidogo tu, tunaitwa PWD, wanapoandika Mheshimiwa Chair waondoe L kwasababu hatutaki jina hili.

Watu walio tafuta kazi walemavu ni 12 na kuna wale ambao hawakukamilishakuleta barua zao. Mimi mwenyewe nafuatilia watu sita kati yao kuna mtu ametafuta kutoka 2013 na akapata wakati huu. Nashukuru bodi ya sasa na pia C.O wa Bodi ya uajiri kwa kuwa rafiki kwetu sisi

kama walemavu. Ananizungumzia kila wakati na kunieleza vitu ambavyo watu wangu wanahitajika kuleta wakitafuta kazi na pia yale hawana. Ninamskia Mandago kule Uasin Gishu alipoandika watu akisema kuwa kama hakuna mlemavu irudishwe. Nakushukuru mwenyekiti kwa sababu yetu leo linafanana kuwa watu sita wameandikwa kihalali na wanfunza shule hii. Wa sita ni kasoro kidogo na ataajiriwa wakati mwingine na nimtafutie barua aandikwe. Pia waislamu wameandikwa wawili mmoja Baragoi and mwingine hapa, napongeza hao sana, wamefanya kazi nzuri, asante.

**Specially Elected MCA,** (Hon. Lekirenyei Sarah): Asante Mheshimiwa Spika. Ningpenda pia kuchukua nafasi hii kupongeza kamati ya Labour kwa kazi nzuri wamefanya nikiwa mmoja wao; tumehakikisha kuwa mabadilisho yanafanyika ambayo ni kumi na nane, walio staafu ni kama kumi na wanne wameaga dunia. Ukiangalia nambari 11 ni mimi Eunice Lekirenyei nilikuwa Elbarta lakini sasa ni mwakilishi wadi mteule. Wamefanya vizuri kwa muda mrefu tumesukuma hao walimu wapate nafasi hizo. Walimu waliopata nafasi hizi wamefurahi pamoja na jamii nzima. Elbarta walimu waliostaafu ni wanne hivi na mimi pia lakini nikapata nafasi hii namshukuru mungu. Shule hizo wamekaa bila walimu kwa muda mrefu kwasababu ya ajira lakini tunashukuru Kaunti yetu kwa kusikia wito na kubadilisha walimu hao, asante Mheshimiwa Spika.

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Hon. Leerte.

**MCA Porro Ward,** (Hon. Leerte Patrick): Ahsante Bw. Spika Nimesimama kwa sababu leo Porro Wadi iko kati ya Wadi nyingine. Hata leo inaonekana tumeshinda 001 (*laughter*). Kwa hivyo, ninashukuru sana kamati ya Leba ukiangalia mbinu imetumika wakati huu mimi binafsi ninaweza sema wamejaribu, kama kitu ni nzuri tunasema ni nzuri yale tu ningependa kusema katika wadi ya Porro kuna watu waliaga na wale waliretire na ninafikiri ndio tumeweza kupata share kubwa kidogo.

Jinsi ambavyo mheshimiwa Esther amesema ninafikiri kila wadi wana walemavu, na ingekuwa vizuri kama waajiriwe kwa wadi, kila wadi iwe na mlemavu kwa kuwa wengi ninawajua wale ambao wamefanya masomo ya chekechea na hawakufaulu. Sijui tungetumia mbinu gani ili wawe na share yao isiwe kwa jumla, kwa mfano Maralal ni wadi kubwa. Ingekuwa vizuri kila wadi watengewe nafasi moja.

Ni vizuri tungekuwa na walemavu kumi na watano badala ya sita. Hatutakl kuharibu maneno nzuri lakini wakati mwingine tuangalie walemavu waajiriwe kutoka kwa wadi, ili tuweze kuwasaidia wengine waliosomea ujuzi ya shule za chekechea. Walijaribu tangu mwaka wa 2018 Porro wapo wawili au watatu ambao hawajafaulu.

**Specially Elected MCA,** (Hon. Lenamatiyio Silapia): ahsante sana Bw. Spika, ningeomba niweze kuzungumza kwa lugha ya kimombo, lakini ninaona unasema Kiswahili tu..

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Kiswahili tu

**Specially Elected MCA,** (Hon. Lenamatiyio Silapia): Asante sana Bw. Spika, nami pia Nimesimama nikimpongeza Mwenyekiti wa Leba, kwa kazi wameweza kufanya na kuleta ripoti hii kujibu Statement ya Mheshimiwa Lenolkulal Esther, nikijaribu kuangalia kwa hii orodha wanasema ni ya mwaka wa 2024 kwa wale ambao walifaulu.

Ukijaribu kuangalia orodha ya majina hayo ya mwaka 2024 ambayo iliweza kutoka Januari tarehe 30 ya mwaka wa 2025 ambayo tuliona kuwa kulikuwa na marekebisho imeweza kufika katika kitabuhiki imeweza kusema ni 54 lakini Bw. Spika mimi nina ile majina shortlisted ECD teachers ambayo ilifanyika ilikuwa replacement ya 2024 na orodha hiyo ilitoka tarehe 31 Januari na wale ambao wameweza kufaulu ni 52 sio 54 jinsi imeandikwa kwa hii karatasi.

Kuajiri watu kazi inapaswa kuwa kwa uwazi, iwapo list iwe shortlisted na iwe kwa watu wote lakini ukiangalia ile ilikuwa kwa public na yenye imetoka kwa ofisi kuna tofauti maana ile ilikuwa public ni 52 na hii hapa ni 54. Ninaweza sema kwa wale waliweza kufaulu 2024, majibu ambayo yameletwa si sahihi na ni vizuri kuwa Department ingeweza kuwa wazi wangetoa chapa zile successful list waweke kwa public.

Ya pili, kuna orodha ambayo imefika mia tatu na kitu ambayo imeonyesha wale ambao waliweza kuapply kazi. Ukiangalia nambari 198 utakuta kuna mwanadada anaitwa Jane Wanjiku Kariuki, mwalimu huyu ametoka Ngilai na ameajiriwa mwaka 2016 na ukiangalia hapa yupo katika orodha hii ya kazi juzi na hakuwa amefaulu yeye ni mwalimu wa ECD kaunti ya Samburu, hilo ni swali la pili ninaona katika orodha hii.

La tatu Bw. Spika, the issue of 2025…

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Order endelea kwa Kiswahili tafadhali

**Specially Elected MCA,** (Hon. Lenamatiyio Silapia): Mr. Speaker protect me because, unifunike tu kwa sababu lugha hiyo inakuwa tatizo kwangu lakini nitajaribu. Kwa wale ambao waliweza kufaulu mwezi wa pili mwaka wa 2025 ni hamsini, na hatukuon ashortlisting yeyote iliyokuwa kwa public.

Mimi ninaweza uliza ni nini haswa tuna evidence hawa walimu wameweza kuajiriwa, kwa sababu wamekuwa hata wameweka shule ambazo hao walimu wameajiriwa waende wafanye kazi pia ingekuwa evidence hawa hamsini wameweza kupata kazi na wanafanya kazi. Kwa sababu wakaazi wa Samburu hawajui orodha hii imetoka wapi ni vizuri kamati ya Leba waweze kufuatilia watuambie orodha hii tutaweza vipi kukubali kuwa hii ni orodha official. Ingekuwa kwa public na sahihi ya CEO of the Public Service Board, those are my concerns according to the response. Thank you Mr. Speaker but next time consider those of us who does not know Kiswahili.

**Mwenyekiti Kamati ya Leba,** (Hon. Leleruk James): asante Bw. Spika ninataka kumpongeza Waheshimiwa kwa sababu ya kuweza kuona ya kwamba kazi hii ni wazi. Kuna jambo moja Mheshimiwa Silapia ameuliza ya kwamba kuna mwalimu mmoja ambaye ameajiriwa upande ya Ngilai ninataka kusema hivi wale ambao unaona nataka kumpongeza CEO wa Leba kwa sababu tangu aingie ni mtu ambaye anahusisha kila mtu jambo ambalo linaendelea.

Kwa kuwa kati ya hawa waheshimiwa wako hapa mimi nikiwemo mmoja wao kwa wale wanasema kwamba orodha ya watu hamsini ni kwa sababu ya kutoweka kuwa waliofanya mtihani na wote wanatosha kazi 332. Lakini pesa kidogo ilipoweza kupatikana ikasemekana tena kwa sababu ninataka kusema jambo moja Bw. Spika kwamba wale hata ambao wameajiriwa hapa kwa kila Wadi ambayo waheshimiwa wanaweza dhibitisha ni kwamba kuna wale wamekaa miaka mingi, hadi mwingine alikuwa amebakisha karibu miaka tano azeeke lakini bodi hii iko kwa sasa walijaribu kuangalia hata wamendika miaka walimu wako nayo na ukiona karibu miaka ya kufanya kazi inaisha.

Orodha ambayo iliwekwa hakuna jinsi ingeweza kuwekwa nyingine walichukua wale kulingana na nambari na ndio sababu ninakuambia mimi kama mwenyekiti Nimeona kw aorodha ile ya watu hamsini nimepata nafasi mbili.

(*Point Order from Hon. Silapia*)

**Specially Elected MCA,** (Hon. Lenamatiyio Silapia): Thank you Mr. Speaker, I just want to put it clearly that…

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Kiswahili…

**Specially Elected MCA,** (Hon. Lenamatiyio Silapia): ningependa kueleza Mheshimiwa Leleruk ambaye ameleta majibu haya kuwa nimeuliza lile jina kuwa 198 kwa sababu amekuwa mwalimu ambaye ameajiriwa na serikali ya kaunti mwaka wa 2016 lakini ukiangalia katika orodha hii, ukiangaliajinsi walivyosema walisema wale ambao waliapply kazi hii mwaka wa 2024. Jina lake bado limeandikwa, nilikuwa naelezea kuwa jina hili halipaswi kuwa hapa kwa sababu yeye ni mfanyikazi ambaye ni mwalimu wa shule ya chekechea na amekuwa kwa miaka hizo zote, haingekuwa inatokea kwa hii orodha, asante.

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Mheshimiwa Silapia kidogo tu Mheshimiwa Leleruk…

**Mwenyekiti kamati ya Leba,** (Hon. Leleruk James): Bw. Spika Unajua nafasi ambayo anaangalia huyu ambaye ameajiriwa ni mtu ambaye ametoka Nyeri, ukiangalia na pia ningependa Bw. Spika ajue watu wanatumia majina inayofanana, kama ni jambo hili moja uko nayo tunaweza kwenda kwa ofisi ufuatilie lakini isiwe ni jambo ambalo linawezafanya orodh ahii yote ambayo imeandikwa… imeandikwa Nyeri wewe ukiapply kazi katilka Samburu Kaunti orodha itatoka ya kila mtu ambaye ameajiriwa, na huwezi ajiri kazi kama hujandikwa permanent. Kwa hivyo, ni kusema tu kwa wale ambao wameajiriwa watu hamsini, kwa kila Mheshimiwa yuko hapa mimi saa hizi naweza dhibitisha ya kwamba wale amnbao wameandikwa kwa orodha ya watu hamsini tayari wanasomesha, ninataka kudhibitisha kuwa hao walimu 50 na 54 wote wameajiriwa.

**Specially Elected MCA,** (Hon. Osman Dube): Bw. Spika ukiangalia jina vile Mheshimiwa Silapia amesema iko kasoro. Ukiangalia majina lina jina la mama mwislamu ambaye anaitwa Saadia na Fatuma wa Baragoi tukakubaliana sisi na CEO tukasema Saaadia ana kazi iondolewe, alipata kazi Nairobi. Walakini wakati watu waliapply yeye akaaply tena labda alitaka kurudi nyumbani, CEO akakaa nasi tukamweleza huyu amepata kazi ampe Fatuma Abdi wa Baragoi. Labda sasa Bw. Spika ni jambo kama hilo linaweza kuwa kasoro kidogo kidogo.

**Specially Elected MCA,** (Hon. Nakinyi Jane): Thank you Mr. Speaker Sir, nilikuwa ninataka kujibu pia yale Silapia amesema, ukiangalia orodha hii…

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Hon. Jane Order, refer her as Honorable

**Specially Elected MCA,** (Hon. Nakinyi Jane): Okay Hon. Speaker,

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Not Speaker but Hon. Silapia

**Specially Elected MCA,** (Hon. Nakinyi Jane): Okay Hon. Silapia, alisema kuwa kuna jina ambayo imetokezea katika hiyo orodha na ningeunga mwenyekiti mkono, kwa kusema kuwa watu hutumia majina sawa, ukiangalia orodha hiyo ya applicants ambao walifaulu kufanya interview ukiona nambari 206 imeandikwa Jane Lemongi na tunaweza kuwa tu somo, nilikuwa napeana mfano nikasema kuwa mimi nilishangaa nilipoona hapa lakini Kipande ni nambari kidogo na pia miaka ni ndogo,kwa hivyo tunawezakuwa somo, asante.

**The Speaker,** (Hon. Lenamarle Stephen): Wacha tumpe nafasi Mheshimiwa Lenolkulal Esther ndio tupate kufunga

**Specially Elected MCA,** (Hon. Lenolkulal Esther): Asante sana Bw. Spika, Leo nimefurahia Sana Kwa sababu Mheshimiwa Spika wacha hawa waheshimiwa akina Silapia wasikie ile kitu tunasikia wakati wanakoroga kingereza. Nafikiri hii statement yangu undo ya kwanza kurudishwa yenye imeninifurahiosha Sana kati ya yote ile nimeuliza Kwa hii Nyumba. Ningepongeza Chair wa labour, na uyo kijana anaitwa Moses kwa sababu wakati nilikuwa natetea apewe kazi nilikuwa najua ni kijana mchapa kazi.

Kama kuna makossa, tumeona hawa walimu wameajiriwa Kwa Wards. Kwa hivo kila Mheshimiwa ataangalia majina yale yameandikwa pale kwa ziko kwa Ward yake. Na kama watu walikuwa wanaajiriwa hivi wakiwa wqanapewa shares kwa Wards, nafikiri ata hatuna complains kwa hii Nyumba. Tunaomba pia watu wengine wakiandikwa, tupewwe Kwa ma wards ndio complains yetu itakuwa zimeisha. Pia maendeleao zingine kama za maendeleo zigawanywe kwa wards, nafikiri tutaenda bila kuongea sana. Nikiwa mwenye hii statement, nimefurahia na nimeridhika kwa sababu wamama wamepata wamepata kazi ana pia walemavu wameajiriwa. Thank you.

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Asante. Nafikiri wacha tufunge iyo Kwa sababu kitu ikiwa mzuri basi ni mzuri. Hon. Mmbers, pursuant to standing order 53(1), (2) and (3) Members can make general statements on topical issues that;

1. The standing order number 33 (hours of the meeting), the Speaker shall interrupt the business of the County Assembly every Tuesday just before the adjournment to facilitate Members to make general statements on topical issues concerns.
2. A Member who wishes to seek leave to raise a matter under, this standing order shall before 12 o'clock, the day the statement is to be made, hand to the Speaker a written notification of the matter but the Speaker shall refer the request to the County Assembly House Business committee unless satisfied, that the matter maybe properly discussed from the County Assembly.
3. No Member making a statement under this standing order shall speak for more than 3 minutes unless with the permission of the Speaker.

Hon. Lorunyei you have 5 minutes.

**MCA Nachola Ward,** (Hon. Lorunyei Lawrence): Thank you Hon. Speaker, pursuant to standing order 53(2), I beg to make a general statement on topical issues regarding the establishment of the village councils. According to the County Assembly act, there is an office of village council and since we join this House, it has not been implemented. We have asked several times on these statements and we are being also disturbed by village councils back at the village. I want us to come into a conclusion. It is just a concern on when are we going to put this statement into a conclusion. Thank you, Mr. Speaker.

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Members you can discuss, those who want to discuss the same. Hon. Silapia now you can speak English.

**Specially Elected Member,** (Hon. Lenamatiyio Silapia): Thank you Hon. Speaker, let me take this opportunity to thank the Hon. Lorunyei for seeing a gap the administrations within the County government from the office of the governor to the village level. Those village elders have been given by the legal framework of the County and also in the national level to have the village elders within our villages for the betterment of service delivery within our County.

We have been allocating money to recruit village elders for the last years but up to today we did not see any selections or recruitment of the same and that is why today the Hon. Member for Nachola Ward raised that statement. I think this is an argent matter as well as a concern matter of

the day that we are here for three years without village elders within our wards. I think this is a gap between the executive and the electorate.

The same issue is failing our people to get the information about the executive or how County is carrying out their duties on the same way. Having a village elder like a place in Ngilai, he is the one who communicate to the village and making them aware on what is going on in the County. Also activities that are being carried out in the Country and also report to the village administrator of the same village who then reports to the Ward administrator where he reports to the County administrator.

The County administrator also reports to the office of the governor. It is our responsibility to put our inputs to make sure that we cannot allocate budget and nothing is being done. Also my question, where is that budget going if there is no that office in place to be recruited for the last three years? Thank you Hon. Speaker.

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Hon. Leerte.

**MCA Porro Ward,** (Hon. Leerte Patrick): Asante Sana Mheshimiwa. Mimi pia nimesimama kuunga mkonon yale Mr. Lorunyei Mmeber ya Nachola ameuliza. Village elders iko katika katiba ya County. Na mahalin nimetoka, majina ya village elders iliandikwa January an ikaletwa Kwa ofisi husika. Mpaka wa leo bado ziko huku kwa director wa adminstartion.

Sijui ni nini inangojewa na vile Mheshimiwa Silapia amesema kwamba tumekyuwa tukiweka budget na majina haziko, hizi pesa zinanatumikanga na njia gani? Lakini mimi najua pesa ya serikali huwa hazipotei, mimi kama mwakilishi wa porro Ward, ningependa tuepewe haya majina kwa sababu ni mzuri zije hapa ata sisi tuone kwa sababu kama majina zimetoka kwa Ward, hakuna siri, tuletewe tuone. Ni mzuri iyo iwe public iwe document ya hii Nyumba. Asante.

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Hon. Sarah

**Specially Elected Member,** (Hon. Lekirenyei Sarah): Asante Mheshimiwa Spika. Pia mimi nimesimama kuunga Mkono Mheshimiwa Lorunyei wa Nachola Ward kwa kazi mzuri amabayo amefikiria vizuri kwa sababu tumengojea kwa Muda mrefu village elders waweze kuletwa katika nyumba hii ya sheria. Lakini Kwa tumetegea na hatuoni. Katika kijiji, wale wazee pia wanangoja

na pia majina zifikishwe hapa nab ado hatuoni. Tunapenda Nyumbani, tunauliza na tunashindwa tutajibu nini. Asante Mheshimiwa Speaker.

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Hon. Lemantaan.

**MCA Waso Ward,** (Hon. Lemantaan Kelvin): Thank Hon. Speaker, I raise to congratulate Hon, Lorunyei for asking these questions. I think we all understand that the names village councils have been collected from the Ward level. Like in my Ward, Waso Ward, I think there is a first list that was done on January, 2023 and then recently on August there was another list maybe Hon. Speaker through your guidance, we will seek someone in charge to come to the House and explain to us. Thank you.

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Hon. Esther.

**Specially Elected Member,** (Hon. Lenolkulal Esther): Asante Mheshimiwa Spika. Nimesimama pia kuunga mkono Mheshimiwa Lorunyei. Hii maneno nin kama imekuwa vikwazo huku mashinani. Tunaona Miaka zinaenda. Pia wale wansema bado hawajalipwa juuu walikuwa na byudget ana kwanini hawajaliopwa. Tunapenda kujua chida ni nini hasa kwa nini majina hazitoki. Asante Mheshimiwa Speaker.

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Chairman Labour.

**Chairman Labour, MCA Suguta Mar Mar Ward,** (Hon. Leleruk James): Thank Mr. Speaker, I also rise to thank the Hon. Member for Nachola Ward for bringing this issue. Mr. Speaker, I think you will give us guidance because I know the village councils that we have been waiting is under my committee but it is good that we are discussing as a whole House.

I think you can give us direction on the way to go since the Member for Nachola has been asking this question several times and last time we were told the village elders will start from January. There is a rumors that the names have been collected and as the representatives of the people, I know we will have a say on those names but it is good you give directions so that next week maybe we get a feedback. I will go to the concern office and I will bring the Report. Thank you.

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Hon. Minority Leader, our standing orders does not allow us to discuss rumors and therefore we cannot take one as something that we can discuss. Hon. Members, village elders is a very important component of the County government. It

bridges the gap between the executive and the village and they are very crucial and therefore I order Hon. Leleruk to meet the Country secretary, get the information and next week Tuesday 2:30pm, and give us the status of the village council. We want to finish this issue because we have been discussing it for a long time. Thank you.

## ADJOURNMENT.

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): Hon. Members the time being 1 minute past four o'clock and there being no any other business, this Assembly now adjourns until Wednesday 21st May, 2025 at 9:30am.